BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 27 Februari, 2019.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Mohammed Said Mohammed:

Hoja ya Mjumbe Kuhusu Maombi ya wananchi wa Jumuiya ya waendesha Boda boda Zanzibar kuhusu kupatiwa fursa ya kuendelea na kazi ya kusafirisha abiria ili kujipatia kipato.

Mhe. Mohammed Said Mohammed:

Hoja ya Mjumbe Kuhusu maombi ya baadhi ya wananchi wa Unguja na Pemba kuhusu suala la usafiri wa Meli baina ya Visiwa vya Unguja na Pemba.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

118. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Hivi karibuni Baraza la Manispaa wametumia gharama kutia kifusi katika viwanja vya Malindi na Mchangani vilivyopo mkabala na Manispaa yenyewe. Lakini cha kushangaza muda mfupi tu eneo hilo limechimbika lote na Mheshimiwa Naibu Waziri alisema ndani ya Baraza hili kifusi kilichotumika ni cha jiwe wakati si kweli.

(a) Je, eneo hilo lilitiwa kifusi hicho lini hadi leo hii kuwa njia hiyo haipitiki.

(b) Je, kwa nini eneo hilo lisitiwe lami wakati eneo hilo linazalisha karibu shilingi 2,000,000/- kwa mwezi.

(c) Je, ujenzi wa eneo hilo ulitolewa zabuni (tender) au ulifanywa na Baraza la Manispaa.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

95. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kwa kuwa katika hatua za awali za utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa kutumia njia ya miripuko na mitetemo ulishafanyika, na kwa sababu zipo athari zilizojitokeza za uharibifu wa mali ambazo zingehitajika kulipwa fidia kwa wananchi wetu kwa Unguja na Pemba.

(a) Je, Wizara inachukuwa hatua gani ya kufanya tathmini ili kubaini athari ambazo zimejitokeza kutokana na utafiti huo.

(b) Je, ni athari gani za kimazingira ambazo zimeanza kubainika na hatua gani zimechukuliwa kukabiliana na athari hizo.

111. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati.

Kwa kuwa Idara ya Upimaji ililipima na kugawa viwanja eneo la Minyenyeni mwaka 2013, na kwa sababu wapo watu waliolipa hati za viwanja vya eneo hilo na baadae likazuiliwa kwa sababu ilisemekana kwamba ni eneo la shamba la Wakfu.

(a) Je, ni nini hatma ya wananchi hao waliokubaliwa kupewa viwanja na kulipia hati na hadi leo hawajapatiwa viwanja vyengine.

(b) Je, ilikuwaje eneo hilo lipimwe hadi ligaiwe viwanja ndio lijitokeze swali hilo la kwamba eneo hili ni la Wakfu.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

.

45. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Serikali imekuwa na mpango endelevu wa kilimo cha mpunga hasa cha umwagiliaji, na kwa sababu yapo mabonde ambayo hayakauki maji kwa muda wote na kwa sababu hiyo husababisha trekta kushindwa kuyalima jambo ambalo linawafanya kutumia nguvu nyingi na muda mrefu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia "power tiller", “rice planting” au mashine nyengine ndogo ndogo ambazo wakulima wa mabonde ya Kinyakuzi, Mshashani na Kwapape ambayo yana wakulima wengi na kuna sehemu kubwa ya mabonde hayo hayalimiki kwa kutumia trekta.

(b) Je, ni lini Wizara watawajengea miundo mbinu mipya wakulima wa mabonde hayo ambayo miundombinu

yake yote imeshaharibika kutokana na kuchakaa kwa sababu imekuwa ya muda mrefu sasa.

69. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Serikali inachukuwa juhudi za kuleta maendeleo ya kilimo Zanzibar, lakini sijaona juhudi zilizochukuliwa za kulima matunda yaliyokuwa adimu kupatikana Zanzibar wakati madaktari wanatusisitiza tule kwa wingi matunda hayo ili kuimarisha afya zetu.

(a) Je, ni kweli kwamba matunda mengi Zanzibar yakiwemo “apple”, zabibu na mengine hayaoti.

(b) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa za kuotesha mazao ya matunda adimu ambayo asili yake sio Zanzibar.

(c) Je, Serikali haioni sasa umefika muda wa kushajiisha wakulima kulima mazao ya matunda ambayo hayapo Zanzibar.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:</u>

19. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kuna tatizo la taa za kuongozea barabarani katika kisiwa cha Pemba hasa maeneo ya Chake Chake Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Machomane “junction” na Wete Hotel. Katika maeneo hayo hayatumii taa za kuongezea barabarani.

(a) Je, Serikali ina mpango gani kwa maeneo hayo kuwawekea huduma ya taa za kuongozea vyombo vya barabarani.

(b) Je, kama ina mpango huo, ni lini taa hizo zitawekwa.

78. MHESHIMIWA MASOUD ABRAHMAN MASOUD (Jimbo la Bububu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika uongozi wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Rais Aman Abeid Karume alitoa ahadi ya kuitengeneza barabara iliyotoka Barabara kuu ya Dole kuelekea Ndunduke kwa kiwango cha fusi. Kwa bahati barabara hiyo imepangiwa fedha za kuitengeneza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019. Hata hivyo, hadi sasa barabara hiyo haijaanza kutengenezwa wala kuzungumzwa kwamba itafanyiwa matengenezo.

(a) Je, barabara hiyo imepangiwa kiasi gani kuifanyia matengenezo kwa kiwango cha fusi.

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kuifanyia matengenezo barabara hiyo.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa baadae kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

IV. HOJA YA MJUMBE:

Mhe. Mohammed Said Mohammed:

Hoja ya Mjumbe Kuhusu Maombi ya wananchi wa Jumuiya ya waendesha Boda boda Zanzibar kuhusu kupatiwa fursa ya kuendelea na kazi ya kusafirisha abiria ili kujipatia kipato.

Mhe. Mohammed Said Mohammed:

Hoja ya Mjumbe Kuhusu maombi ya baadhi ya wananchi wa Unguja na Pemba kuhusu suala la usafiri wa Meli baina ya Visiwa vya Unguja na Pemba.

Zanzibar,
27 Februari, 2019.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.